REPUBLIC OF KENYA

PACS

OFFENDERS CAN CHANGE



# MPANGO WA AMRI YA HUDUMA KWA JAMII NCHINI

# KIJITABU

WWW.PROBATION.GO.KE

# KUTUHUSU

**MPANGO WA A**MRI YA HUDUMA KWA JAMII NCHINI KENYA

Mpango wa amri ya Huduma kwa jamii ni hukumu isiyohusisha kifungo cha jela, ambapo mhalifu anayestahili kufungwa kifungo cha miaka isiyozidi mitatu gerezani huamrishwa kutoa huduma ya bure (bila malipo) kwa umma badala ya kufungwa gerezani. Kazi hii ni sharti ifanywe kwa manufaa ya jamii. mhudumu haruhusiwi kufanya kazi katika maskani au kikao cha mtu binafsi. Baadhi ya miradi ambayo wahudumu huamrishwa kutekeleza ni kama upanzi wa miti ili kuanzisha misitu; ujenzi wa nyumba na barabara, udumishaji usafi katika nyanja za umma na mitaa, utunzaji visima vya maji na kadhalika. Wataalam kama vile walimu, madaktari, waashi na waseremala wanaweza kupewa kazi katika shule, hospitali na vituo vya ujenzi.

**NI NANI ANAYEPASWA KUPATA HUKUMU HII YA AMRI YA HUDUMA KWA JAMII?**

Mkosaji anayemudu kutoa huduma kwa jamii ni yule ambaye hatia yake haizui tetezi za umma au kustahili kifungo cha zaidi ya miaka mitatu. Wakosaji wa wizi kutumia nguvu, kunajisi, makosa ya kujamiiana na umilikaji wa madawa ya kulevya hawafai kuhusishwa katika utaratibu huu. Mhalifu ni sharti awe na makao ya kudumu, na awe tayari kutoa huduma kwa jamii na kufuata masharti ya utaratibu huu.

**MPANGO HUU UNA MALENGO YAPI?**

Mpango huu umekusudia:

- Kuondoa msongamano magerezani na kupunguza gharama kwa serikali.
- Kuhusisha jamii katika urekebishaji tabia ya wakosaji.
- Jamii kupata fidia kwa hasara aliyosababisha mkosaji kupitia kwa huduma ya miradi kwa jamii.
- Huhakikishia familia na jamii ya mhudumu amani huku akiendelea na kazi zake za kawaida za ujenzi wa taifa.

# USIMAMIZI WA MPANGO

**MPANGO HUU UNA USIMAMIZI WA JINSI GANI?**

Mpango huu unasimamiwa na kamati ya kitaifa ya huduma kwa jamii chini ya uenye kiti wa jaji wa mahakama kuu. Mpango wenyewe hutekelezwa kupitia kwa kamati kuu ya kitaifa ambayo katibu wake ndiye mratibu wa kitaifa wa huduma kwa jamii.

Mratibu wa kitaifa ndiye afisa mkuu wa mpango huu. Bali na huyu mratibu wa kitaifa kuna maofisa wa huduma hii katika mahakama kote nchini ambao hutekeleza wajibu huu. Kila mahakama ina kamati ya uongozi ambao mwenyekiti wake ni hakimu na katibu wake akiwa afisa wa huduma kwa jamii.

Wanakamati katika kuhusishwa na kamati kuu ya kitaifa; mahakama na jamii. Mpango wa huduma huu kwa jumla huelekezwa na mahakama huku ukitekelezwa na kamati kuu pamoja na Idara ya Probesheni kwa manufaa ya umma.

**MAJUKUMU YA KAMATI KUU NI YAPI?**

Kamati kuu ndiyo shirika tekelezi na majukumu yake ni Kama ifuatavyo:

- Usimamizi wa uendeshaji wa ofisi ya utekelezi.
- Ukusanyaji, uhifadhi na usambazaji wa tarakimu.
- Kushauri kamati zote za huduma kwa jamii kuhusu sera zilizoundwa na kamati ya kitaifa.
- Kuelimisha na kuhamasisha umma na watekelezaji haki dhidi ya uhalifu kuhusu madhumuni ya mpango huu.
- Kushirikiana na mashirika mengine katika maswala yanayohusiana na mpango huu.

# FAIDA YA MPANGO HUU

**AFISA WA ARMI YA HUDUMA KWA JAMII NI NANI?**

Afisa wa huduma kwa jamii ni afisa wa mahakama aliye na majukumu yafuatayo:

- Kutayarisha na kutoa ripoti ya kabla ya hukumu mahakamani.
- Kutambua mahali pa kazi panakofaa kwa kila atakayewekwa kwa mpango huu.
- Kusimamia kazi na kukadiria mafanikio ya wahudumu.
- Kuhakikisha kuwa sheria za amri ya kuhudumia jamii zinatimizwa.
- Kuomba mahakama ichunguze upya hukumu huduma ya wahudumu kwa jamii.
- Kuwezesha upatanisho kati ya wahudumu na jamii.
- Kulinda wanaohusika na mpango huu dhidi ya ubaguzi.
- Kutotambua siri za wahudumu.
- Kuhifadhi kumbukumbu na kukadiria kiasi cha utekelezaji kazi na wahudumu.
- Kuwasilisha mara kwa mara ripoti kuhusu wahudumu kwa kamati ya huduma za kwa jamii zinazohusika.
- Kushirikisha shughuli za kamati za mpango huu pamoja na mahakama kuhusiana na utaratibu huu.

**MSIMAMIZI WA MIPANGO HUU NI NANI?**

Msimamazi hapa ni yule mtu ambaye anasimamia mhudumu katika mahali pake pa kazi. Huyu ndiye mkuu wa taasisi anayoitumikia mfungwa. Yeye hutekeleza kazi yake chini ya maelekezo ya afisa wa huduma kwa jamii. Hata hivyo, yeye pia hapati ujira wowote kwa kazi hii.

**FAIDA YA MPANGO HUU NI IPI?**

- Inapunguza gharama kwa serikali.
- Inamfunikia mhudumu fedheha ambayo angepata akiwa gerezani.
- Inamwepusha kutokana na wahalifu ambao ni sugu (wamekuwa wagumu kurekebishwa).
- Ni njia ya kiutu ya kurekebisha tabia ya mhalifu.
- Husaidia kuondolea mbali msongamano magerezani.
- Huhusisha jamii katika kurekebisha tabia ya wahalifu.
- Hufidia waliotendewa mabaya.
- Husaidia kutambua na kutumia ujuzi na maarifa ya wahalifu kwa manufaa ya jamii.
- Inamwezesha mhudumu kupata ujuzi wa kazi

# MASHARTI YA HUDUMA

### HUDUMA HII INA MASHARTI GANI?

Kuna masharti ambayo wewe ukiwa mhudumu unapaswa kufuata ukielekezewa na afisa wa huduma kwa jamii na usimamizi wa mwangalizi wa huduma hii. Masharti hayo ni kama ifuatavyo:

- Kufanya kazi ulivyoagizwa kwa njia ya uwajibikaji.
- Kushirikiana na mwangalizi wako huku ukifuata maagizo uliyopewa.
- Kuwa na tabia njema, uaminifu na mwenye kusema ukweli.
- Ufanye kazi nyakati zote na kukaa katika mahali pako pa kazi hadi mwangalizi wako atakapokuruhusu kuondoka.
- Kuripoti kuhusu mabadiliko ya kazi au makazi kwa Afisa wa huduma hiyo au mwangalizi wako.
- Utimize mapatano ya kukutana na afisa wako au mwangalizi wako ili kujadili maendeleo kazini kwako.
- Mabadiliko yoyote ya maagizo yatafanyika tu panapo makubaliano kati yako na afisa wako.
- Usijihusishe na watu waliopotoka kitabia.
- Epuka utumizi wa madawa au vinywaji vya kulevya.
- Ni sharti uishi mahali ambapo afisa wako atakuwa amekushauri kuwa panafaa.
- Masharti mengine yanaweza kuongezeka.

### UPEO WA MPANGO HUU

- Huduma hii inatekelezwa nchini kote na imeleta ufanisi mkubwa katika nchi yetu ya Kenya. Kila mahakama na afisi ya urekebishaji tabia nchini Kenya ina habari zaidi kuhusu mbinu bora za utekelezaji wa mpango huu.
- Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana na mshirikishi wa kitaifa au afisa yeyote wa urekebishaji tabia au mahakama yoyote nchini Kenya.